KUSIKILIZA, KUZUNGUMZA NA KUSOMA - CBC GRADE 2 TERM 3 EXAMS 2023

SEHEMU YA A:

SEHEMU YA 1:

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu asome mwanafunzi ajibu maswali

Asubuhi na mapema tuliitwa na mama. Anga ilikuwa shwari. Jua lilikuwa limechomoza. Mama akatuambia twende tukapatie ng'ombe nyasi na maji na tufungulie kuku. Mama alitutayarishia kiamsha kinywa. Tulikunywa uji kwa viazi tamu.

1. Hali ya anga katika hadithi ilikuwa? _____
2. Jua huchomoza wakati gani? _____
3. Chakula cha asubuhi huitwa? _____
4. Ni wanyama wangapi wametajwa kwa hadithi? _____
5. Ng'ombe hukula _____

SEHEMU YA 2:

KUSOMA KWA SAUTI

Jina langu ni Nyaganya. Ninasoma katika gredi ya pili. Niko mfupi na mnene. Mimi ninajua kusoma Kiswahili. Mimi hubeba vitabu na kalamu kwenye mkoba.

Mwalimu wangu wa darasa anaitwa Bwana Nyongesa.